



Maombi ya kujiunga na Jopo la Washauri Vijana wa UNFPA.

Utangulizi

UNFPA tunaamini kuwa uwekezaji kwa vijana ni mkakati madhubuti wa kuweza kufikia Malengo Endelevu ya Dunia (SDGs) pamoja na maazimio ya Mkutano wa Kimataifa wa Idadi ya watu (ICPD).

Vijana wana maono na mitazamo inayoweza kupelekea sera na mipango madhubuti ili kuhakikisha malengo na mipango yaliyowekwa na serikali inafikiwa. Hivyo sisi UNFPA hatuna budi kutengeneza mazingira rafiki ya uwezeshaji kwa vijana. Moja ya mikakati yetu ni kuhamasisha uongozi kwa vijana na ushiriki wao katika kufanya maamuzi kupitia mpango wetu wa kuwa na jopo la washauri vijana ambalo liliundwa toka mwaka 2006 kama njia mojawapo ya kuwapa nafasi vijana kushiriki kikamilifu katika kupanga, kusimamia na kufanya maamuzi juu ya program za UNFPA zinazowalenga vijana.

Kupitia jopo la washauri, vijana wana nafasi ya kutoa maoni, kuchangia mawazo na kushauri UNFPA na wadau wengine juu ya ushiriki wa vijana katika utekelezaji wa malengo endelevu ya dunia hapa Tanzania.

Hivyo UNFPA, inaitisha maombi toka kwa vijana 15 toka Tanzania bara na Zanzibar ili kuwa wanachama wa jopo la vijana kwa kipindi cha mwaka 2021-2023. Vijana watakaofanikiwa watasajiliwa kama wanachama wa jopo la washauri vijana wa program za UNFPA.

Majukumu

Wanachama wa Jopo la washauri vijana watakuwa na majukumu yafuatayo.

1. Kubadilishana elimu na taarifa kuhusu mafanikio ya utekelezaji wa sera na mipango mbalimbali inayowahusu vijana, kupeana habari juu ya fursa na changamoto zilizopo katika kuendeleza agenda za maendeleo ya vijana, ikiwemo masuala ya usawa wa kijinsia, afya ya uzazi na haki kwa vijana.
2. Kuzungumza kwa niaba ya vijana wenzao, kutetea na kufanikisha ushirikishwaji wenye tija kwa vijana katika majukwaa ya utungaji wa sera na mipango mbalimbali.
3. Kuwezesha uelewa mpana baina ya UNFPA, Serikali, vikundi vya vijana na wadau mbalimbali juu ya sera na mipango ya UNFPA na jinsi gani vijana wanaweza kufikiwa katika nyanja tofauti za kisiasa, kijamii na kitamaduni.
4. Kushauri UNFPA, Serikali na wadau wengine juu ya kuhakikisha ushiriki wenye tija wa vijana katika kutunga sera, mipango na kazi zote zilizomo katika maeneo ambayo UNFPA inafanyia kazi.
5. Kushiriki katika majukwaa mbalimbali ikiwemo yale yanayofadhiliwa na UNFPA katika ngazi za kitaifa Kikanda na Kimataifa yanayoratibu agenda za maendeleo ya vijana kama vile usawa wa kijinsia na afya ya uzazi kwa vijana.

6. Kutambua masuala mtambuka yanayowahusu vijana kwenye eneo la afya ya uzazi na haki ikiwemo masuala ya ujinsia, mila na desturi.
7. Kutoa taarifa juu ya changamoto za vijana kama vile usawa wa kijinsia, maambukizi ya virusi vya ukimwi na haki za vijana katika ngazi tofauti kikanda na kitaifa, majimbo na jamii kwa ujumla.
8. Inapobidi, kushiriki katika vikao na warsha mbali mbalimbali zinazoandaliwa na UNFPA na wadu wengine, vikiwemo vikundi vya kitaalamu na mipango mbalimbali.

Taratibu za kazi: Ni kazi ya Kujitolea kwa kipindi chote cha miaka 3 (2021- 2023)

SIFA za Mwombaji

- a. Awe na umri kati ya miaka 15 hadi 22.
- b. Awe na ufahamu wa masuala ya Malengo Endelevu ya Dunia (SDGs), uongozi kwa vijana, ushiriki wa vijana, haki za binadamu na usawa wa kijinsia.
- c. Awe tayari kufanya kazi katika mazingira yoyote ikiwemo kufanya kazi na vijana wenye maono tofauti na ya kwake.
- d. Awe na utambuzi wa mambo na uwezo wa kujisimamia.
- e. Awe na uwezo mzuri wa mawasiliano na kuchangamana na wengine
- f. Awe na utayari wa kufanya kazi kwa ushirikiano na wengine
- g. Awe na ujuzi wa kutumia kompyuta pamoja na mitandao ya kijamii.
- h. Awe tayari fanya kazi kwa kujitolea angalau kwa masaa 16 ndani ya wiki katika kipindi cha uanachama wake.

Lugha: Kiswahili. Ajue kuzungumza na kuandika. Kujua kiingereza ni sifa ya ziada.

Uzoefu:

- Mshiriki mahiri katika masuala yote ndani ya jamii yake hususan yale yanayo husu maendeleo ya vijana
- Awe mwanachama wa taasisi au kikundi chochote cha vijana katika jamii yake kama vile taasisi za kidini, taasisi zinazo shughulika watu wenye ulemavu, taasisi zinazofanyia kazi masuala ya elimu, michezo, ujinsia, uongozi, mendeleo vijijini na masuala ya ukimwi.

Mshahara

- Uanachama wa jopo la vijana ni kazi ya kujitolea, hakuna malipo yoyote yatakayotolewa wa ajili ya kazi hiyo.
- UNFPA italipia gharama zote zitokanazo na safari Pamoja na malazi endapo mwanachama atahudhuria vikao au warsha mbalimbali zinazohusiana na uanachama wake.

Jinsi ya kuomba

Kwa wale watakaopendezwa wanatakiwa kuwasilisha yafuatayo:

- Barua ya motisha
- Nakala ya wasifu wako (CV)
- Barua ya utambulisho kutoka katika taasisi ambayo wewe ni mwanachama



Maombi yote yatumwe kwa anuani zifuatazo: thassan@unfpa.org kwa ajili ya Tanzania bara na kheri@unfpa.org kwa Zanzibar . Mwisho wa kuwasilisha maombi ni tarehe **20/12/2020.**

Ukihitaji ufafanuzi zaidi tafadhali wasiliana na thassan@unfpa.org au kheri@unfpa.org

Baada ya tarehe ya mwisho ya kutuma maombi mawasiliano yatatolewa kwa wale watakao fanikiwa kuchaguliwa, endapo hautasikia chochote kutoka kwetu baada ya wiki mbili kutoka tarehe ya kufunga tangazo, basi ufahamu kuwa haukufanikiwa

UNFPA ni Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu ambalo lina malengo la kuwa na Dunia ambayo kila Mimba inahitajika, Kila Uzazi ni Salama, na kila lengo la Kijana linafikiwa.

UNFPA inatoa kipaumbele juu ya usawa ikilenga vijana walio katika makundi maalum hususan wale walio katika mazingira magumu na waliotengwa wakiwemo vijana wenye ulemavu na vijana wanaoishi na VVU.